Jina…… **Nambari Yako……..…**

102/2 **Sahihi ……..**
KISWAHILI
Karatasi ya 2 **Tarehe……..**
LUGHA
Julai/Agosti, 2011
Saa: 2½

MTIHANI WA KAMATI YA KUIMARISHA ELIMU KATIKA JIMBO LA BARINGO 2011

Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Saa: 2½

Maagizo:
(a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Jibu maswali yote.
(c) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali

Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	**15**	
2	**15**	
3	**40**	
4	**10**	
	Jumla	

1. **UFAHAMU**

Msingi mkuu wa shughuli ya uhakiki ni kuwepo kwa kitu cha kuhakiki. Msingi huu unaelekeza kwenye nafasi ya mtunzi au mwandishi katika harakati za uhakiki. Uhakiki ni zao la usomaji wa makini ambao umekitwa kwenye mazoea, misingi ya kitaaluma, urazini na utumiaji wa akili.

Suala la kuwepo kwa mwandishi na mhakiki linatuelekeza kwenye mjadala kuhusu mambo mawili ya kimsingi kumhusu mtunzi au mwandishi wa kazi ya kifasihi. Kwanza, pana uhusiano wa aina gani kati ya mtunzi/mwandishi na mhakiki wa kazi ya kifasihi? Pili, mhakiki ana nafasi gani katika uendelezaji wa fasihi kama taaluma? Je, kuwepo kwa mhakiki kuna umuhimu gani katika historia ya uhakiki au taaluma nzima ya uhakiki. Baadhi ya maswali haya yana msingi ya kifalsafa.

Uhusinao uliopo kati ya mwandishi na mhakiki umekuwa chanzo cha mvutano mkubwa. Mjadala huu umekita kwenye mvutano wa kujaribu kutathmini mchango na labda hata umuhimu wa mhakiki katika ukuaji na uendelezaji wa fasihi. Baadhi ya waandishi huwaangalia wahakiki kama vimelea ambao hutegemea kuwako kwa kazi ya kifasihi ili kuhalalisha shughuli na taaluma zao, na kwamba, asilimia kubwa ya uhakiki wao unalenga kufichua dosari za kazi ya kifasihi – zilizopo na labda hata za kudhaniwa. Wahakiki wengine kwa upande wao hushikilia kuwa mhakiki ana uwezo wa kuelekeza uandishi kwa kiasi kikubwa.

Baadhi ya mikabala ya uhakiki imekitwa kwenye imani kuwa mhakiki ana nafasi kubwa kwa kuwa anamsaidia msomaji kuielewa kazi fulani inayohusika. Mikabala ya kirasimi ya kumhusu mhakiki humwangalia kama mwalimu na mfafanuzi ambaye anafafanua sifa za kifani na za kimaudhui za kazi Fulani inayohusika na kuifanya ieleweke vyema. Msimamo kama huu umejengwa kwenye mtazamo wa kumwangalia mhakiki kama kielelezo cha ufahamu unaoupita ule wa mwandishi – anayeweza kuelewa mambo yote kuihusu kazi ya kifasihi. Huu ni mkabala ambao unapotosha kwa kiasi kikubwa kama anavyoeleza Mario Vargas Llosa.

Uhakiki ulivyo wenyewe, hata pale unapokuwa wa makini na undani na uliochochewa na kariha hauwezi kuelezea au kufafanua fennmena ya ubunifu katika ukamilifu wake … bunilizi nzuri au shairi aali litakuwa na element ambazo au mkabala ambao uchanganuzi wa kihakiki unashindwa kuelezea … uhakiki ni zao la akili (na mazoea) na werevu … ubunifu kwa upande wake unatokana na uhisia, silka nguvu zisizoweza kuelezeka na hata sadifa. (Letters, 133)

MASWALI

(a) Uhakiki ni nini? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(b) Kwa nini baadhi ya waandishi huwaangalia wahakiki kama vimelea? (alama 4)

_____

_____

_____

_____

(c) Urasumi unasema nini kuhusu mhakiki kulingana na kifungu hiki? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(d) Mkabala wa kirasimu umechukuliwa kuwa wa kupotosha. Kwa nini? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(e) Fafanua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa katika kifungu. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa na mwandishi. (alama 3)

(i) Urazini _____

_____

(ii) Silka _____

_____

(iii) Sadifa _____

_____

2. **<u>UFUPISHO</u>**

Huenda nyakati ambazo wanaharusi walikuwa wakizingatia utaratibu wa dini au jamii zao kubadilishana viapo vya ndoa zikafikia ukingoni huku watu wengi wakiamua kujiandikia viapo vyao wenyewe wakati wa sherehe za arusi. Kwa wakati huu, idadi kubwa ya wachumba wanachagua kuandika viapo vyao wenyewe kinyume na enzi za awali ambapo wapenzi walikuwa wakifuata viapo vilivyowekwa kama kanuni na dini zao. Imebainika kuwa mabadiliko ya wakati na kuporomoka kwa mila na tamaduni za baadhi ya jamii kumechangia hali hii.

Baadhi ya sababu zinazotolewa kuhusu hali hii ni kuwa dunia imebadilika mno huku watu wengi wakielimika wala sio kwamba ni kupotoka. Eti ni dunia ambayo watu wanahitaji uhuru wa kujiamulia mambo na kwamba ndoa kama taasisi muhimu, inafaa kuachiwa wahusika kujiamulia mambo wenyewe ikiwa ni pamoja na kubadilishana viapo vyao wakati wa harusi.

Kufuata kanuni za kidini au kimila kuliwanyima wapenzi fursa ya kuelezea hisia zao kikamilifu kwani walinakili-tu yaliyokuwa yameandikwa na wengine. Dini nyingi na madhehebu huwataka wafuasi wao kukariri viapo vilivyoandikwa na ambavyo vimekuwepo kwa miaka mingi, mtindo ambao hauwavutii wengi siku hizi. Wanasema kuwa kuandika na kuvisoma mbele ya wageni wakati wa harusi kunaongeza ladha ya huba. Hata hivyo, baadhi ya dini zinazoshikilia kwa dhati kanuni za harusi haziwakubalii wafuasi wao kuandika na kuvisoma viapo vyao wenyewe. Jambo hili huwafanya waumini wasiokubaliana na msimamo huu kufunga ndoa chini ya usimamizi wa viongozi wa serikali.

Kizazi cha sasa kinatamani sana uhuru wa kujieleza na hakifai kunyimwa fursa hiyo. Kuwanyima fursa ya kujielezea ni ukandamizaji lakini sharti wakati wa ushauri, wanandoa wafafanuliwe viapo vyao ili viapo vyao vizingatie muktadha wa taasisi ya ndoa. Mtindo huu wa wachumba kuandika viapo vyao umeshika kasi miongoni mwa wachumba walioelimika na unaashiria mabadiliko makubwa katika ndoa.

MASWALI

(a) Kwa kutumia maneno baina ya **40-45**, fupisha aya ya kwanza na ya pili. (alama 7)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

(b) Fupisiha aya ya tatu na ya nne kwa maneno **55-60**. (alama 5)

NAKALA CHAFU

NAKALA SAFI

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) **Ainisha viambishi** vya awali na vya tamati katika neno lifuatalo: Waingiamo. (alama 2)

(b) (i) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi ‘ongopa’. (alama 1)

(ii) **Tambulisha** aina za **nomino** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Umma katika Jamhuri yetu unataka haki ya kila mja itekelezwe.

(c) **Unganisha** sentensi hizi kwa kutumia **kirejeshi** cha kati. (alama 2)

(i) Mpira umepotea
(ii) Mpira ni wangu.

(d) Andika katika **usemi halisi**.

Kiptoo alimwambia shangazi yake kuwa angekuwa akienda kumtembelea kwake kila wiki. (alama 3)

(e) Yakinisha katika **wingi**.

Hakukuarifu kuhusu yule hajala. (alama 2)

_____

_____

(f) Fafanua kwa kutungia sentensi **matumizi** mawili ya neno **namna**. (alama 2)

_____

_____

_____

(g) **Pambanua** sentensi ifuatayo kwa kutumia kielezo cha **jedwali**. (alama 4)

Kalamu mpya ni ya mwalimu.

_____

_____

_____

_____

(h) Vinyambue vitenzi vifuatavyo kulingana na maagizo. (alama 2)

(i) Ja _____ (tendwa)

(ii) La _____ (tendesha)

(iii) Nata _____ (tendeshwa)

(iv) Juvya _____ (tenda)

(i) Tunga sentensi **moja** ili kudhirisha matumizi ya viwakifishi hivi:

Mdokezo, mshazari. (alama 2)

_____

_____

(j) (i) Eleza nini maana ya **mofimu**. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

\

(ii) Bainisha aina za **mofimu** katika maneno yafuatayo.

Lakini
Kiti (alama 2)

_____

_____

_____

(k) Eleza maana **mbili** katika sentensi hii. (alama 2)

Majambazi walimwibia Letangule gari jipya.

_____

_____

_____

_____

(l) **Unda** vivumishi kutokana na vitenzi hivi. (alama 2)

(i) Dhalilisha _____

(ii) Thibiti _____

(m) Fafanua **tofauti** kati ya kirai na kishazi. (alama 2)

_____

_____

_____

(n) (i) Taja sauti mbili za kaakaa laini. (alama 1)

_____

(ii) Taja irabu za. (alama 1)

_____

(o) Andika katika hali ya **udogo**:

Mvulana yule alibeba kiti kikubwa. (alama 2)

_____

_____

(p) Fafanua matumizi ya kwa, ki na po katika sentensi ifuatayo.

Walipokuwa wakilima waliimba kwa furaha. (alama 3)

(q) Andika kwa **wingi**.

Mimi ndimi shangazi yake. (alama 1)

4. **ISIMU JAMII**

(a) Eleza nitazamo mitatu kuhusu chimbuko la Kiswahili huku ukionyesha ikiwa matazamo huo una mashiko au la. (alama 6)

(b) Fafanua dhima ya lugha ya Kiswahili hapa nchini. (alama 4)